

Jiunge nasi katika Siku ya Ndege Wanaohama Duniani 2014!



'Maeneo ndege hupitia wakihama: Ndege wanaohama na Utalii'

World Migratory Bird Day

10-11 Mei 2014

Kuambatana na kauli "Maeneo ndege hupitia wakihama: Ndege wanaohama na Utalii" (Destination Flyways: Migratory Birds and Tourism), Siku ya Ndege Wanaohama Duniani (WMBD) 2014 itaonyesha uhusiano kati ya hifadhi ya ndege wanaohama, maendeleo ya jamii na utalii kote duniani.

Kila mwaka, zaidi ya watalii bilioni moja huvuka mipaka ya kimataifa. Kama vile wanyamapori ni rasilmali yenye thamani, mhamo wa ndege inayosisimua pia ni ya thamani kubwa katika sekta ya utalii. Shughuli za kitalii zinazohusika na ndege wanaohama (kwa mfano kuwatazama au kuwapiga ndege picha) zikisimamiwa vizuri zinaweza kuwa msingi thabiti wa kuleta faida katika uhusiano baina ya watu na ndege wanaohama.

Katika kampeini ya mwaka 2014, WMBD ikishirikiana na UNWTO (Shirika la Kimataifa la Utalii) itatilia mkazo njia ambazo ndege wanaohama hufuata katika misimu...kwa kingereza 'Maeneo ndege hupitia wakihama'. Ikiongozwa na UNWTO pamoja na mashirika mengine yenye ujuzi na utaalamu katika nyanja za utalii na hifadhi ya mazingira, 'Maeneo ndege hupitia wakihama' inanuia kukuza utalii unaostawi katika maeneo ambayo ndege hao hutua wakati wa safari zao zinazojulikana katika kingereza kama 'Flyways'. Kwa kutumia mapato kutoka utalii, mpango huu unanuia kuyalinda makao ambayo ndege hawa hutua katika safari zao, wakati huo huo ukiwapa wakaazi wa maeneo hayo ajira zinazohusiana na hifadhi ya mazingira. Katika kampeini ya mwaka huu wa 2014, 'Maeneo ndege hupitia wakihama' itakuwa mfano maalum ya jinsi utalii inayohusika na ndege wanaohama inaweza kuwa chombo cha utunzaji wa mazingira na ustawi wa jamii kwa kuleta faida kwa wanyamapori, wakaazi wa maeneo hayo na pia watalii.

Siku ya Ndege Wanaohama ni nini?

WMBD ilianzishwa mwaka 2006 lengo lake likiwa kusositiza na kutilia mkazo hifadhi ya ndege na ulinzi wa mazingira yao ulimwenguni. Kampeini hii inapangwa katika mifumo miwili ya mikataba ya kimataifa: Shirika la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira (UNEP) – Mkataba wa Hifadhi ya Wanyama Wanaohama (CMS) na Mkataba inayohusika na ndege wanaohama baina ya Africa, Ulaya na Asia (African-Eurasian Migratory Waterbird Agreement -AEWA). UNWTO na mashirika mengine mengi yanazidi kujiunga kuifadhili kampeini ya mwaka huu 2014.

Jiunge nasi na kushiriki katika Siku ya Ndege Wanaohama duniani itakayokuwa tarehe 10-11 Mei 2014. Ikiwa utaamulia kuchangia katika siku hii – aidha kwa kuandaa matukio ya kuwatazama ndege, mafunzo kuhusu ndege wanaohama, kuhutubia miadhara, maonyesho ya picha na mengine mengi – kila shughuli itachangia kampeini hii duniani.

Jifunze mengi zaidi kuhusu Siku ya Ndege Wanaohama Duniani! Sajili onesho lako na kuitisha picha, stika au kadi bila gharama katika tovuti ya WMBD (www.worldmigratorybirdday.org) na upate kuonyesha ulimwengu nzima jinsi umechangia siku ya WMBD 2014.

Tutafurahia kusheherekea Siku ya Ndege Wanaohama 2014 pamoja nawe!

Kwa maelezo zaidi au kuagiza picha, tafadhali tuandikie:

Ms Dunia Sforzin, UNEP/AEWA Secretariat

Tel: +49 (0)228 815 2454

Fax: +49 (0)228 815 2450

E-mail: contact@worldmigratorybirdday.org